# KATIBA

# YA

# CHAMA CHA

# DEMOKRASIA MAKINI

# YA JUNI, 2000

**TOLEO LA 2015**

( Toleo hili la Katiba ya Chama Cha Demokrasi MAKINI linajumuisha marekebisho yote ya Katiba ya 2000 tokea ilipoanza kutumika mwezi Juni mpaka tarehe 20 Juni, 2015)

**24th May, 2016**

## YALIYOMO


UTANGULIZI ..... 3
JINA, NEMBO NA BENDERA ..... 4
MISINGI YA KISIASA YA CHAMA ..... 5
MADHUMUNI YA CHAMA ..... 6
UANACHAMA ..... 8
HAKI ZA MWANACHAMA ..... 8
WAJIBU WA MWANACHAMA ..... 8
KUONDOKA AU KURUDI KATIKA CHAMA ..... 9
SIFA ZA KIONGOZI KATIKA CHAMA ..... 9
MIIKO YA UONGOZI ..... 11
HAKI ZA UONGOZI ..... 11
KUACHA UONGOZI ..... 12
VIKAO VYA CHAMA ..... 12
VIKAO VYA VITONGOJI/MTAA/SHEHIA ..... 12
VIKAO VYA TAWI/SHEHIA ..... 13
MKUTANO MKUU WA TAWI/SHEHIA ..... 13
VIKAO VYA KATA/WADI ..... 16
VIKAO VYA JIMBO/WILAYA ..... 19
VIAKO VYA WILAYA/MKOA ..... 22
VIKAO VYA TAIFA ..... 25
VIONGOZI WAKUU WA CHAMA. ..... 29
MWENYEKITI ..... 30
MAKAMU MWENYEKITI ..... 30
KATIBU MKUU ..... 31
NAIBU MAKATIBU WAKUU ..... 31
WAGOMBEA WA KITI CHA URAIS ..... 32
VITENGO VYA CHAMA ..... 33
NAFASI ZIKIWA WAZI ..... 37
BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA ..... 37

MAREKEBISHO YA KATIBA........................................ 38
KANUNI ZA CHAMA........................................ 38
KUVUNJA CHAMA........................................ 39

## KATIBA YA CHAMA CHA DEMOKRASIA MAKINI

## SEHEMU YA KWANZA

### UTANGULIZI

1.1 Kwa kuwa Chama cha demokrasi MAKINI ni Chama cha siasa ya Kidemokrasia kitokanacho na kiu ya watanzania kujiletea maendeleo ya hakika, haraka nay a kweli katika misingi ya kujitegemea, usawa, Umoja na kuheshimu utu;

1.2 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa elimu bora. Hasa katika sayansi ya teknolojia, ndiyo njia pekee ya kuleta maendeleo yay a uhakika nay a kweli kwa jamii ya Watanzania.

1.3 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa ubinafsi uliokithiri kuwa chanzo kikubwa cha matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali za umma, kwa pamoja zikiwa ndiyo kisa cha umaskini wa Tanzania, licha ya bahati kubwa Taifaletu lililopata ya kuwa na watanzania wenye busara , kwa mfano baba wa Taifamarehemu Mwalim Julius Kambarage Nyerere, na rasilimali nyingi, zikiwemo madini, mbuga za utalii, maziwa na mito yenye maji mengi, ardhi safi kwa kilimo, bahari yenye samaki wengi na ufukwe unaopakana nan chi yetu kwa Zaidi ya urefu wa kilomita 800, na bahari ya kupwea misaada mingi na wahisani kwa Zaidi ya miaka 53;

1.4 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa hata nchi zililokuwa masikini kuliko Tanzania miak aya sitini na zilizokuwa na rasilimali chache sana kulinganisha na Tanzania zimepiga hatua kubwa kimaendeleo katika uzalishaji wa kutumia sayansi na teknolojia kiasi cha kujenga uwezo wa kutoa misaada kwa nchi nyingine, hii ikiashiria kuwa nchi yetu ina utajiri na rasilimali za kutosha kukudhi mahitaji ya maendeleo ya jamii yetu iwapo itazingatia uzalishaji wa kutumia sayansi na teknolojia ya kisasa na iliyo rahisi.

1.5 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa Tanzania ilidharau wasomi wa kitanzania na kuwakumbatia wasomi wan je, na hivyo kutowatumia wasom wazalendo ipasavyo kwa maendeleo ya Taifa, na badala yake kuwaachia wasomi wake walio wengi kubabaishwa na wafadhili wa nje kwa maslahi ya nchi za nje, na kwa madhara makubwa kwa Tanzania ya leo na hasa Tanzania ya kesho;

1.6 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa Katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania ina kasoro nyingi zinazokandamiza haki za mtanzania na ambazo zinahitaji marekebisho makubwa ili kuiwezesha Tanzania kujijenga upya kuwa

nchi ya Amani ya kudumu yenye mfumo wa siasa ya demokrasia ya vyama vingi, utawala wa haki unaolindwa na mahakama iliyo huru pamoja na bunge linalotekeleza wajibu wa ke wa kuidhibiti Serikalina kuwajibika kwa wananchi.

1.7 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua umuhimu wa kudumisha Umoja wa Tanzania na kushiriki katika harakati za kuleta muungano wan chi za kiafrika.

1.8 Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinatambua kuwa umuhimu wa uwiano kati ya wanaume na wanawake katika shughuli zote za maendeleo ya jamii.

1.9 Na Kwa kuwa Chama cha demokrasia MAKINI kinaamini kuwa njia pekee ya kulikomboa Taifaletu kutoka katika ufukara na umaskini, na badala yake kujenga Taifatajiri lenye raia wenye afya na maisha mazuri, ni kutoa elimu bora kwa watanzania wote wenye nguvu ya kuyamudu masomo, pamoja na kutumia nguvu kazi ya watanzania wote wenye uwezo wa kufanya kazi;

Hivyo basi, Chama cha demokrasia MAKINI kinawasilisha Katiba hii ya Chama inayotokana na mtazamo wa Chama.

## SEHEMU YA PILI

### JINA, NEMBO NA BENDERA

2.1 JINA: la Chama litakuwa Chama cha demokrasia MAKINI, kwa kifupi MAKINI likiwa na maana ya maarifa kilimo na nishati.

2.2 Nembo ya MAKINI ni mduara uliogawanya sehemu tatu, sehemu ya juu ikiwa na picha ya trekta ndani ya rangi ya kijani, sehemu ya kati na kati ikiwa na mikono miwili iliyoshikana ndani ya rangi nyeupe, na sehemu ya chini ikiwa na miraba saba, kila mmoja ukiwa na rangi moja wapo kati ya urujuani, nili, buluu, manjano, machungwa, nyekundu na nyeusi.

**2.3 BENDERA YA CHAMA:** itakuwa na rangi kuu tisa. Itakuwa na trekta ndani ya rangi ya kijani kushoto, mikono miwili iliyoshikana ndani ya rangi nyeupe katikakati, na miraba saba, kila mmoja ukiwa na rangi moja wapo urujuani, nili, buluu, manjano, machungwa, nyekundu na nyeusi, kulia. Trekta ina maana ya kilimo cha kisasa, mikono iliyoshikana ina maana ya Amani, na rangi saba zina maana ya matumizi ya sayansi na tekinolojia kwa maendelelo ya watanzania wote. Maneno Chama cha demokrasia MAKINI yataandikwa ndani ya rangi nyeupe.

2.4 Michoro ya vielelezo vya nembo ya MAKINI na bendera ya Chama iko mwishoni mwa Katiba hii yah Chama.

2.5 MAKAO MAKUU ya Chama yatakuwa mjini **Dar es Salaam.**

2.6 AFISI KUU itakuwa **Zanzibar.**

## SEHEMU YA TATU

## MISINGI YA KISIASA YA CHAMA

3.1 kuheshimu haki za binaadamu kwa watu wote popote walipo bila ubaguzi wa aina yoyote.

3.2 Kuendesha shughuli zote za Chama kwa demokrasia ya kweli yenye kuwashirikisha walengwa katika maamuzi na utekelezaji wa maamuzi yote yanayowahusu.

3.3 Kujenga jamii mpya ya kitanzania katika misingi ya kuheshimu utu, na kuimarisha Amani, usawa, haki ya kufanya kazi na kupat kipato cha kutosheleza mahitaji muhimu ya maisha, haki ya kupata elimu, haki ya kuapta ardhi, haki ya kufanya shughuli yoyote ya kimaendeleo ndani ya sharia popote Tanzania. Haki ya kutokuota ama kupokea rushwa, haki ya mtanzania yoyote kumiliki mali na haki ya kuabudu katika dini anayopenda.

3.4 Kujenga mahusiano bora na nchi zote duniani, yatakayowawezesha watanzania kusafiri kwa urahisi ili kufanikisha ushrikiano wa kibiashara na kitaalam kati ya watanzania na watu wan chi zote ndani ya sharia za kimaTaifakwa lengo la kujiletea maendeleo ya kibinafsi na Kitaifa.

3.5 Kufuata mfumo wa siasa ya kujitegemea, hii ikiwa ni pamoja na kulinda mali za watanzania zibaki mikononi mwa watanzania, na zisichukuliwe na wajanja wachache kutoka ndani au nje ya Tanzania.

3.6 Kushirikisha watanzania wote waliowanachama wa MAKINI, bila ubaguzi, kwenye shughuli za Chama.

3.7 Mwenyekiti wa Chama katika ngazi ya uongozi atakuwa na kura ya turufu ambayo itatumika iwapo kura za wajumbe zitafungana baada ya kuradiwa mara tatu.

3.8 Kumteua aliyepata theluthi mbili ya kura zilizopigwa kuwa mshindi katika chaguzi kwenye ngazi yoyote ya Chama, isipokuwa kama mshindi hatapatikana baada ya kupiga kura mara mbili basi aliyepata kura nyingi Zaidi atakuwa mshindi, na kama kura zitafungana baada ya kurudiwa mara tatu, Mwenyekiti wa kikao katika uchaguzi husika atutumia kura yake ya turufu kuchagua mmoja wa wagombea walioshikamana kuwa mshindi.

3.9 Kupitisha maamuzi yote ya vikao vya Chamayasioyokuwa ya uchaguzi kwa kura ya asilimia 51 ya wajumbe wote wa kikao husika wenye haki ya kupiga kura.

3.10 Kuendesha shughuli zote za Chama kwa kuzingatia ushauri utakaotolewa na kamati ya wataalam wa Chama pale inapowezekana. Hususan kamati hizo zitachaguliwa kutoka miongoni mwa wanachama wenye busara katika ngazi husika, akiwemo Mwenyekiti na katibu wa Chama katika ngazi hiyo.

## SEHEMU YA NNE

**MADHUMUNI YA CHAMA**

4.1 Kushehimu, kulinda na kutekeleza haki za binaadamu popote walipo.

4.2 Kujenga utamadauni wa kuheshimu na kutmia demokrasia katika maamuzi yote yanayowahusu watu.

4.3 Kuhakikisha kuwa lengo la shughuli zote za Chama na Serikaliyake,ndani na nje ya nchi, ni kuboresha maisha yamtanzania na jamii ya watanzania kwa ujumla.

4.4 Kuboresha na kulinda heshima ya mtanzania popote alipo duniani kote.

4.5 Kutenga nafasi zisizopungua theluthi moja ya nafasi zote za uongozi pale inapowezekana, katika ngazi zote za Chama na Serikaliya Chama cha MAKINI kwa ajili ya wanawake wenye uwezo, lengo likiwa ni kufikia uwiano wa asilimia hamsini.

4.6 Kuboresha mazingira na kutokomeza uharibifu wa Mazingira sehemu zinazokaliwa na watu na zile zisizokaliwa na watu.

4.7 Kujenga na kuimarisha utamaduni wa vyombo vya dola kuheshimu utu katika kutekeleza majukumu yake ndani ya sheria, hii ikiwa ni pamoja na kushirikisha bunge kisheria kaitka uteuzi wa wakuu wa vyombo vya dola pale ambapo Katiba ya nchi inaruhusu. Na utamaduni wa watu binafsi, mashirika na makampuni kufanya shughuli zao ndani ya sharia ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

4.8 Kuhimiza matumizi ya sayansi na teknolojia katika njia zote za uzalishaji ili kuimarisha na kukuza uchumi wa Taifa, hii ikiwa ni pamoja na kukutumia pato la Taifakwa maendeleo ya watanzania, na kukaribisha wawezekaji watakaozalisha kwa soko la ndani na la nje.

4.9 Kufanikisha uingizaji wa teknolojia mpya kutoka pande zote za dunia kwa lengo la kuwawezesha watanzania wabunifu na wenye vipaji kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania.

4.10 Kuimarisha soko la ndani na soko la nje, hii ikiwa ni jitihada maalum ya kuwaondolea hasa wakulima kero ya kuzalisha mazao na kukosa soko. Hususan soko la ndani litalindwa, vyama vya ushirika vitaimarishwa na wakulima watashauriwa na kusaidiwa kuanzisha vyombo vyao vya fedha pale inapowezekana.

4.11 Kulinda kisheria mali za mtanzania yoyote alizozipata kihalali ndani na nje ya nchi.

4.12Kuwadhamini watanzania wasio na uwezo wa kujidhamini katika vyombo vya fedha, pale inapowezekana, lakini wenye uwezo wa kuzalisha mali ama kutoa huduma mbalimbali za kijamii, ili wapatiwe mikopo na vyombo vya fedha ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujenga uwezo wa watanzania kutumia uwezo wao wa kiutendaji kuimarisha uchumi wao na uchumi wa Taifa, na hivyo kuondoa ukiritimba wa watu

wachache kuwa matajiri katika jamii ya maskini wengi, licha ya kwamba hata hao maskini wana vipaji sawa na hao matajiri, na licha ya kwamba hakuna mtanzania anayependa umasikini.

4.13 Kupinga kisheria ubaguzi wa aina yoyote kwa misingi ya dini, rangi, kabila, jinsia na uchumi, hii ikiwa ni pamoja na kuKataza uwekezaji wa vitega uchumi vyenye mwelekeo wa kuwabagua watanzania, kwa makusudi, kwa kisingizio chochote kile.

4.14 Kuwa na bunge huru na lenye wabunge walio sawa kwa maana ya kufanya kazi ya ubunge kikamilifu, na lenye mamlaka ya kuidhibiti serikali, hii ikimaanisha kuwa wabunge hawatakuwa watumishi wa serikali, isipokuwa pale Katiba ya nchi inapolazimisha, lengo likiwa ni kuwawezesha kufanya kazi zao za ubunge kwa ufanisi Zaidi, na kuondoa upendeleo wa serikali, unaosababishwa na wabunge Fulani kupewa madaraka mengine, na usiokuwa wa lazima katika kutoa huduma zake kwa wananchi.

4.15 Kuheshimu na kulinda uhuru wa mahakama

4.16 Kuheshimu, kulinda, kukuza na kutumia utaalamu wa kitanzania, hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa kazi yoyote iliyoko ndani ya uwezo wa watanzania itafanywa na watanzania kisheria bila kujali mfadhili wa kazi hiyo, isipokuwa tu pale ambapo ufadhili wa kazi hiyo sio mkopo, lengo likiwa ni kupinga ukoloni mambo leo, kulinda ajira ya watanzania na kuepuka mikopo ya kiini macho ambayo kwa hakika haina manufaa kwa nchi yetu, na badala yake inatuongezea umasikini.

4.17 Kukaribisha wahamiaji wenye teknolojia kutoka pande zote za dunia, na kujenga mazingira mazuri yatayowashawishi wataalam wa kitanzania wasikimbilie nchi nyingine kwa lengo la kutafuta mazingira bora zaidi, hii ikiwa ni pamoja na kuwashawishi wataalam wa kitanzania waliokimbilia nje kurudi Tanzania.

4.18 Kuhakikisha kuwa elimu itolewayo Tanzania ni ya ubora wa kimaTaifa, na yenye uwezo wa kutambua na kukuza vipaji na utundu wa aina zote ili kumuwezesha kila mtoto wa kitanzania kubobea katika fani anayoipenda.

4.19 Kuhakikish akuwa elimu na tiba ni haki ya kimsingi ya mtanzania kwa maana ya kuwa elimu kwa wote na afya kwa wote ni jukumu la jamii, isipokuwa wenye uwezo kiuchumi watagharamia gharama zote zinazohusu familia zao, wenye uwezo mdogo watalipia gharama inayolingana na uwezo wao, na wasio na uwezo kabisa watapata huduma hizo bila malipo.

4.20 Kujenga mfumo wa uchumi wa kujitegemea, hii ikiwa ni pamoja na kukaribisha wawekezaji watakaozalisha kwa ajili ya masomo ya ndani nje, na hivyo kulingiizia Taifafedha za kigeni, kujenga mazingira yatakayowawezesha watanzania kuweka vitega uchumi nchi za nje kwa ajili ya kuboresha uchumi wa Tanzania, na kuzilinda mali za watanzania zisiporwe na wajanja wachache kutoka ndani na nje ya Tanzania. Hususan wawekezaji wageni ambao hawatazalisha fedha za kigeni kwa ajili ya kuendesha vitega uchumi vyao hawatakaribishwa.

4.21 Kutumia mbinu za kisayansi ili kuhakikisha kuwa Serikaliiliyo madarakani, iwe ya Chama cha MAKINI ama ya Chama kingine, inatawala nchi kwa sera zilizoiweka

madarakani, na si kinyume cha sera hizo, kwani kutekeleza kinyume cha sera hizo ni kuvua uhalali wa Serikalihiyo kutawala.

## SEHEMU YA TANO

### UANACHAMA

5.1 Raia yoyote wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi ana haki na uhuru wa kuwa mwanachama wa Chama cha MAKINI, isipokuwa ni lazima alipe ada ya kila mwaka ya uanaChamakamaitakavyopangwa na kamati kuu ya Taifamara kwa mara.

5.2 Raia yoyote anayetimiza kipengele 5.1 ataruhusiwa kuwa mwanachama cha Chama cha MAKINI iwapo atakiri kukubaliana na madhumuni, sera, itikadi na kanuni za Chama, pamoja na kuahidi kuzilinda, kuzitetea na kuzitekeleza kwa muda wote atakaokuwa mwanachama, hii ikiwa ni pamoja na kushiriki katika shughuli za uongozi iwapo atatakiwa kufanya hivyo.

## SEHEMU YA SITA

### HAKI ZA MWANACHAMA

6.1 Kugombea nafasi ya uongozi katika ngazi zote katika Chama na kupigiwa kura wote walio na sifa za kupiga kura.

6.2 Kupiga kura katika uchaguzi wa viongozi katika maeneo husika.

6.3 Kupata habari zote za maamuzi ya vikao vya Chamavinavyomhusu.

6.4Kushiriki kikamilifu katika vikao vya Chamavinavyomhusu.

6.5 Kushiriki kikamilifu katika vikao vya Chamavinavyomhusu, hii ikiwa ni pamoja na kutoa mawazo na kusikiliza mawazo ya washiriki wengine.

6.7Kujieleza na kujitetea mbele ya kamati za Chama pale Ambapo patakuwa na mashitaka ama malalamiko ya aina yoyoteyanayomhusu.

6.8 KuKata rufaa kwa vikao vya juu iwapo muhusika hakuridhika na maamuzi ya vikao vya chini.

## SEHEMU YA SABA

### WAJIBU WA MWANACHAMA

7.1 Kutimiza masharti yote ya uanaChama wakati wote wa uanaChama wake.

7.2 Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za Chama zinazomhusu

7.3 Kutekeleza ilani ya Chama kwa uwezo wake wote, hii ikiwa ni pamoja na kuwa raia mwema, mwenye kupenda na kuboresha maendeleo ya watanzania wote, na mwenye maadili ya kuigwa na watanzania wengine.

7.4 Kuchukia na kukerwa na rushwa

7.5 Kutokutoa ama kupokea rushwa

7.6 Kutokumbatia walarushwa kwa makusudi.

7.7 Kukubali kushindwa au kushinda katika chaguzi zote atakazo shiriki na kukubali matokeo ya chaguzi za Kidemokrasia zitakazokihusisha Chama, isipokuwa pale ambapo chaguzi hizo zitatawaliwa na udanganyifu.

7.8 Kupinga uonevu ama ubaguzi wa aina yoyote ndani nan je ya Chama. Hii ikiwa ni pamoja na kuKataa matokeo ya uchaguzi uliotawaliwa na udanganyifu kama vile wizi wa kura, au uchaguzi suiokuwa huru na wa haki.

7.9 Kudhuria vikao vyote vya Chama vinavyomhusu, kutoa mawazo yake na kusikiliza mawazo ya wenzake.

7.10 Kurejesha kadi ya Chama na dhamana nyingine yoyote itakayokuwa chini yake, na kutorejesha ada au mchango wowote aliotoa kwa Chama, iwapo ataacha kuwa mwanachama.

## SEHEMU YA NANE

## KUONDOKA AU KURUDI KATIKA CHAMA

8.1 Mwanachama ataacha uanachama kwa hiari yake ama kwa kulazimishwa kama ifuatavyo:-

a) Kwa kujiuzulu mwenyewe kwa hiari yake.
b) Kwa kufukuzwa iwapo atathibitika kutotimiza masharti ya uanaChama kwa makusudi
c) Kwa kujiunga na Chama chengine cha siasa.
d) Kwa kutoa siri za Chama nje ya vikao vya Chama bila kuwa msemaji mkuu wa Chama aliyetauliwa rasmi kwa kazi hiyo
e) Kwa kufariki
f) Kwa kufukuzwa iwapo mwanachama atagundulika kuwa anakuhujumu Chama cha MAKINI

8.2 Mwanachama atakaeacha kuwa mwanachama kwa sababu zozote zile atakuwa na haki ya kuomba uanachama upya kwa kuwasilisha barua na kuza fomu maalum katika Tawi/Shehia la Chama.

## SEHEMU YA TISA

## SIFA ZA KIONGOZI KATIKA CHAMA

9.1 Awe na historia ya uchapa kazi na utendaji kazi mzuri wenye kutoa matunda yanayoonekana, ikiwa ni pamoja na kukamilisha kazi wakati unaotakiwa, kufanya kazi kwa muda mrefu bila malalamiko ama madai yasiyo ya msingi, kufurahia kazi nzuri na kuchukizwa na utendaji mbovu wa kazi.

9.2Awe na tabia ya kusikiliza na kutatua matatizo ya watu wa ngazi zote bila ubaguzi, hii

ikiwa ni pamoja na kuyatafuta matatizo ya watu wengine kwa lengo la kuyatatua.

9.3 Awe anachukia umasikini, uonevu, rushwa, ukandamizaji, na tabia nyingine zinazowakera wananchi.

9.4 Awe anapenda maendeleo ya watu.

9.5 Awe anapenda Amani na utulivu.

9.6 Awe mtu asiye na mali iliyopatikana kwa njia ya udanganyifu, wizi, ama unyonyaji wa wanyonge.

9.7 Awe anakemea uzembe kwa nguvu zake zote.

9.8 Asiwe na historia ya uhalifu wa makosa ya jinai

9.9 Awe na tabia ya kuheshimu watu wa aina zote.

9.10 Awe na kiu ya matumizi ya teknolojia ya kisiasa katika uzalishaji wa mali na utoaji huduma.

9.11 Awe na elimu inayolingana ama kupita uwezo unaohitajika na kazi ya uongozi anayotka.

9.12 Awe anajiamini kuwa ana uwezo wa uongozi unaopita wanachama wengine wote wanaotaka uongozi unaohusika.

9.13 Awe anapenda elimu, hii ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya shule na taasisi nyingine zinazotoa mafunzo, na awe anapenda kujiendeleza na kuwaendeleza watu wengine.

9.14 Awe ni mwenye kupanga matumizi bora ya muda wake na muda wa watu wengine.

9.15 Awe ni mtenda haki, mkweli na asiye na ubinafsi.

9.16 Aheshimu viongozi wa serikali, vyama vingine vya siasa, na vikundi vingine vya wananchi kama vile dini, kwa kutumia lugha, hoja na kauli za kistaarabu katika kujadili mambo yanayohusu viongozi, vyama na vikundi hivyo.

9.17 Awe na sababu za kuomba uongozi, hii ikiwa ni pamoja na kuyaelewa mazingira yake, matatizo ya wananchi yanaomkera, na mbinu na ratiba za kuyatatua matatizo hayo.

9.18 Akubali kuwajibika kama itabainika kuwa amewarubuni wananchi pale ataposhindwa kwa makusudi kutoa huduma alizoahidi.

9.19 Asiwe mbadhirifu wa mali za umma, hii ikiwa ni pamoja na kuchukua matumizi ya fedha za umma kununua vitu vya anasa vyenye gharama kubwa zisizoendana na umasikini wa watanzania.

9.20 Awe mtekelezaji na mtetezi wa sera za Chama.

9.21 Asiwe na tabia inayokera jamii.

9.22 Kama ana familia basi ni lazima awe ni mtu aliyetumia uwezo wake kuindeleza familia yake kielimu na vinginevyo.

9.21 Asiwe na tabi ainayokera jamii.

9.22 Kama ana familia basi ni lazima awe ni mtu aliyetumia uwezo wake kuiendeleza familia yake kielimu na vinginevyo.

9.23 Awe ni mtu MAKINI katika kuongoza na kufanya maamuzi.

## SEHEMU YA KUMI

### MIIKO YA UONGOZI.

Katika Chama cha MAKINI, kiongozi ni mwanachama aliye mjumbe katika kamati yoyote ya Chama na vitengo vyake. Ifuatayo ni miiko ya uongozi katika Chama.

10.1 Kiongozi atakayekosa kuhudhuria kikao kinachomhusu mara mbili mfululizo, bila kutoa udhuru ukakubalika, atapoteza haki yake ya kuwa kiongozi.

10.2 Kiongozi atakayopokea ama kutoa rushwa atafikishwa katika vyombo vya sharia haraka iwezekanavyo na atapoteza uongozi wake kama atapatikana na hatia.

10.3 Kiongozi atakayeshindwa kujibu malalamiko/tuhuma kutoka kwa wanachama kuhusu utendaji wake wa kazi, katika muda wa siku thelathini tangu kujulikana hadharani kwa malalamiko hayo ama tuhuma hizo, atapoteza haki yake ya kuwa kiongozi.

10.4 Kiongozi atakayekisaliti Chama, kwa mfano kwa kutoa siri za Chama bila kibali cha maandishi, atapoteza uanachama wake.

10.5 Viongozi wa Chama cha MAKINI wana wajbu wa kuzitetea sera za Chama chao bila kukashifu vyama vingine vya siasa ama vingoziwa seikali iliyoko madarakani.

10.6 Kiongozi atakayetumia mali ya Chama/wananchi kwa ubadhirifu atapoteza haki yake ya kuwa kiongozi.

10.7 kiongozi atakayetuhumiwa kujihujumu , kukidhalilisha amakukiaibisha Chama atapoteza haki yake ya kuwa kiongozi.

10.8 Kiongozi atakayetumia madaraka aliyopewa na Chama kupora mali ya mwananchi/wananchi atapoteza haki yake ya uongozi na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

10.9 Kiongozi atakayehukumiwa na mahakama kwenda jela kwa kosa lisilo la kisiasa atapoteza haki ya uongozi.

10.10 Kiongozi atakayeendesha shughuli za Chama bila kufuata Katibaya Chama na sheria za nchi atapoteza haki yake ya uongozi.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

### HAKI ZA UONGOZI

11.1 Atakuwa na haki ya kujiuzulu

11.2 Atakuwa na haki ya kujitetea mbele ya vikao vya Chama kwa tuhumaa zozote zile zinazomkabili, kwa madhumuni ya kuonyesha ni kwanini asichukuliwa hatua za kinidhamu.

11.3 Atakuwa na haki ya kuKata rufaa kwenye vikao vya juu kama hakuridhika na maamuzi ya vikao vya chini.

11.4 Atakuwa na haki ya kuongoza wananchi waliomchagua ndani ya sharia za nchi, na ndani ya Katiba ya Chama, na kufuata ilani ya uchaguzi ya Chama.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

### KUACHA UONGOZI

12.1 Kwa kujiuzulu kwa sababu zozote zile, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa imani kutoka kwa theluthi mbili ya wajumbe wa kamati ama Halmashauriya ngazi husika.

12.2 Kwa kuachishwa uongozi kwa sababu za kutotimiza masharti ya uongozi.

12.3 Kwa kupoteza uanaChama wake.

12.4 Kwa kumaliza kipindi cha uongozi kilichowekwa na Katiba ya Chama.

12.5 Kwa kubainika kuwa muhusika aliwadanganya wapiga kura wakati wa uchaguzi kwa kiwango kilichosababisha yeye kuchuaguliwa, na kuthibitika kuwa muhusika hangechaguliwa isipokuwa kwa uongo wake wa makusudi.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### VIKAO VYA CHAMA

Kutakuwa na vikao vya Chama katika ngazi zifuatazo.

i) Vitongoji/Mtaa ii) Tawi/Shehia iii)Kata/Shehia iv) Jimbo/Wilaya v) Mkoa vi)Taifa.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE

### VIKAO VYA VITONGOJI/MTAA/SHEHIA

Hivi ni viako vya ngazi ya chini kabisa. Kitongoji/Mtaa/Shehia utakuwa na wanachama wasiopungua kumi. Kitongoji/Mtaa/Shehia utakuwa na vikao vya aina mbili kama ifuatavyo:-

14.1 Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia

Kutakuwa na Mkutano Mkuu mmoja kila mwaka, utakaojumuisha wanachama wote chini ya Mwenyekitiwa Kitongoji/Mtaa/Shehia wa Chama ama mwanachama atakayechaguliwa na Mkutano Mkuuhuo kukaimu nafasi hiyo kwa muda, kwa utaratibu ufuatao:-

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Kitongoji/Mtaa/Shehia wa Chama ambae atachaguliwa miongoni mwa wanachama na Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena.
b) Mwenyekiti wa Kitongoji wa Chama ndiye msemaji mkuu wa Chama na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Chama katika Kitongoji/Mtaa/Shehia
c) Kutakuwa na katibu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia wa Chama ambaye atachaguliwa miongoni mwa wanachama na Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena.
d) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia ni wanachama watano.

e) Wajumbe wa Mkutano Mkuu watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yoyote kukaimu nafasi ya katibu kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.
f) Wajumbe wa Mkutano Mkuu watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

**14.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia.**

a) Kumchagua Mwenyekiti wa Chama wa Kitongoji/Mtaa/Shehia
b) Kumchagua katibu wa Chama wa Kitongoji/Mtaa/Shehia
c) Kudumisha Amani na Umoja katika Kitongoji/Mtaa/Shehia
d) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia
e) Kuhakikisha kuwa kila mwanachama aliye na uwezo wa kufanya kazi anashawishiwa na kusaidiwa ili aweze kufanya kazi kwa lengo la kutekeleza sera ya kujitegemea
f) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia
g) Kuandaa Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia

## SEHEMU YA KUMI NA TANO

**VIKAO VYA TAWI/SHEHIA**

Hivi ni vikao vya ngazi ya pili kutoka chini. Tawi/Shehia litakuwa na wanachama wasiopungua ishirini na tano. Tawi/Shehia litakuwa na vikao vya aina mbili kama ifuatavyo:-

**MKUTANO MKUU WA TAWI/SHEHIA**

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Tawi/Shehia, ambaye atachaguliwa miongoni mwa wanachama na Mkutano Mkuukila baada ya mika mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.
b) Mwenyekiti wa Chama ndiye msemaji mkuu wa Chama na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Chama katika Tawi/Shehia.
c) Kutakuwa na katibu mtendaji wa Tawi/Shehia, ambaye atachaguliwa miongoni mwa wanachama na Mkutano Mkuu kila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.
d) Kutakuwa na mweka hazina wa Tawi/Shehia, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia.
e) Kutakuwa na Mkutano Mkuu mmoja kila mwaka, chini ya Mwenyekiti wa Tawi/Shehia ama mwanachama atakaechaguliwa na huo Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia kukaimu nafasi hiyo kwa mda, na ambao utajumuisha wanachama wafuatao:-
    i. Mwenyekiti wa Tawi/Shehia.
    ii. Katibu mtendaji wa Tawi/Shehia
    iii. Mweka hazina wa Tawi/Shehia
    iv. Wenyeviti wote wa vitongoji/Mtaa iliyoko katika Tawi/Shehia

v. Makatibu wote wa vitongoji/mitaa iliyoko katika Tawi/Shehia.
vi. Wajumbe wawili kutoka katika kila Kitongoji/Mtaa/Shehia watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kitongoji/Mtaa/Shehia unaohusika.

f) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia itakuwa nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 15.1 (e) (i) hadi (iv)

g) Wajumbe Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura za wajumbe waliopo.

### 15.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia

a) Kuchagua Mwenyekiti wa Tawi/Shehia
b) Kupokea ripoti ya utendaji kutoka Halmashauriya Tawi/Shehia, na ripoti ya utendaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maamuzi mbalimbali na mapendekezo pale inapobidi.
c) Kumchagua katibu mtendaji wa Tawi/Shehia.
d) Kumchagua mweka hazina wa Tawi/Shehia.
e) Kuchagua wajumbe watatu wa Halmashauriya Tawi/Shehia.
f) Kuchagua wajumbe wawili watakaowakilisha Tawi/Shehia kwenye Mkutano Mkuu wa Kata/Shehia.
g) Kuhakikisha uhai wa Chama katika Tawi/Shehia.
h) Kupokea ripoti za maendeleo kutoka kwenye kamati za uongozi za vitongoji/mitaa iliyoko katika Tawi/Shehia, na ripoti ya utendaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maelekezo kwa kamti ya uongozi ya kila Kitongoji/Mtaa/Shehia.
i) Kupokea takwimu za wanachama wasio na ajira kutoka Halmashauriya Tawi/Shehia, na kusaidia harakati za kuwatafutia ajira, kuwapa ushauri na kuwapa misaada mingine ya hali na mali pale itakapowezekana wakati wakisubiri kupata ajira.
j) Kutayarisha ripoti ya maendeleo ya wanachama/wananchi, ikionyesha hali halisi ya ajira (walioajiriwa na waliojiajiri) na kipato cha kaya, kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Chama aktika Kata/Shehia husika.
k) Kupokea maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Kata/Shehia
l) Kuwawajibisha viongozi wa Chama katika ngazi za vitongoji/mitaa ambao watapatikana na makossa yanayostahili hatua za kinidhamu.

### 15.2 Halmashauriya Tawi/Shehia

a) Kutakuwa na Halmashauriya Tawi/Shehia itakayokutana si chini ya mara tatu kwa mwaka, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-
i. Mwenyekiti wa Tawi/Shehia.
ii. Katibu mtendaji wa Tawi/Shehia
iii. Mweka hazina wa Tawi/Shehia
iv. Wenyeviti wote wa vitongoji/mitaa iliyoko katika Tawi/Shehia

v. Makatibu wote wa vitongoji/mitaa iliyoko katika Tawi/Shehia.
vi. Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia.
vii. Diwani wa eneo la Tawi/Shehia iwapo ni mwanachama wa MAKINI.

b) Koramu ya mikutano ya Halmashauriya Tawi/Shehia itakuwa na nusu ya wajumbe wa Halmashauriwaliotajwa kaitka kifungu 15.2 (a) (i) hadi (v)

### 15.2.1 Kazi ya Halmashauriya Tawi/Shehia

a) Kusimamia shughuli zote za Chama, kuzitangaza na kuzitetea sera na ilani ya uchaguzi ya Chama, kushawishi wananchi wajiunge na Chama cha MAKINI na kuboresha maendeleo ya wanachama/wananchi katika Tawi/Shehia.
b) Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanachama/wananchi katika Tawi/Shehia.
c) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Kata/Shehia.
d) Kupokea ripoti za mikutano mikuu ya vitongoji/mitaa, na kuthamini maendeleo ya Tawi/Shehia pamoja na kutoa mwelekeo wa baadaye kwa kamati za uongoiz za vitongoji/mitaa.
e) Kudumisha Amani, Umoja na mashirikiano katika Tawi/Shehia.
f) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kiuchumi, elimu, michezo n.k kwa kuwashirikisha wanachama/wananchi wenye kuhitaji huduma hizo
g) Kutoa ushauri na misaada ya aina mbalimbali kwa wanachama/wananchi wenye kuhitaji huduma hizo.
h) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu wa Chama katika Kata.
i) Kuhimiza kila kaya kupeleka watoto shule na kuhimiza wananchi kujiendeleza kielimu, ikiwa ni pamoja na kusaidia pale inapowezekana.
j) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka uliopita, na kutayarisha bajeti ya mwaka ya Chama, pamoja na ripoti za mapato na matumizi ya Chama katika Tawi/Shehia.
k) Kusimamia matumizi bora ya mali ya Chama.
l) Kuunda kamati/idara mbalimbali za kufanikisha malengo ya Chama, hii ikiwa ni pamoja na kuteua wasimamizi wa kamati/idara hizo, na kupanga utaratibu wa utendaji wa kamati/idara hizo.
m) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuboresha demokrasia, hii ikiwa ni pamoja na kufanikiswa chaguzi zote za kidemkrasia kwa kufanya kampeni kwa njia ya amani.
n) Kuhitimisha maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Tawi/Shehia, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya wanachama walio na sifa za kugombea nafasi za uongozi wa Chama katika Tawi/Shehia.
o) Kupendekeza hatua za kinidhamu kwa viongozi wa vitongoji/mitaa kwa ajili ya kufanyiwa uamuzi na Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA

### VIKAO VYA KATA/WADI

Hivi ni vikao vya ngazi ya tatu kutoka chini. Kata/Wadi itakuwa na vikao vya aina mbalimbali

### 16.1 Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Kata/Wadi wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata/Shehia, kutoka mingoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena.

b) Mwenyekiti wa Chama ndiye msemaji Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.

c) Kutakuwa na katibu mtendaji wa Kata/Wadi wa Chama, ambaye atachaguliwa na mkutano wa Kata/Wadi, kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.

d) Kutakuwa na mweka hazina wa Kata/Wadi, ambaye atateuliwa na Halmashauriya Kata/Wadi.

e) Kutakuwa na mweka hazina wa Kata/Wadi, ambaye atateuliwa na Halmashauriya Kata/Wadi.

f) Kutakuwa na Mkutano Mkuu mmoja kila mwaka chini ya Mwenyekiti wa Kata/Wadi, ama mwanachama atakayechaguliwa na huo Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi kukaimu nafasi hiyo kwa muda.

g) Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi utajumuisha wajumbe wafuatao:-

   i. Mwenyekiti wa Kata/Wadi.
   ii. Katibu mtendaji wa Kata/Wadi
   iii. Mweka hazina wa Kata/Wadi
   iv. Wenyeviti wote wa Kata/Wadi yaliyoko katika Kata/Wadi.
   v. Makatibu wote wa Kata/Wadi yaliyomo katika Kata/Wadi.
   vi. Wajumbewawili kutoka katika kila Tawi/Shehia watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi/Shehia linalohusika.
   vii. Madiwani wote walioko katika Kata/Wadi ambao ni wanachama wa Chama cha MAKINI.
   viii. Wenyeviti wa Serikaliza vitongoji/Mtaa walioko katika Kata/Wadi ana ambao ni wanachama wa Chama cha MAKINI.
   ix. Wabunge walioko katika Kata/Wadi na ambao ni wanachama wa Chama cha MAKINI.

h) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Kata,Wadi ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 16.1 (f) (i) hadi (v)

i) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi watakuwa na haki ya kumchagua mwanachamayeyote kukaimu nafasi ya katibu kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

j) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yoyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

### 16.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi.

a) Kuchagua Mwenyekiti wa Kata/Wadi
b) Kuchagua katibu mtendaji wa Kata/Wadi
c) Kupokea ripoti za utendaji na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama kutoka Halmashauriya Kata/Wadi, kuzijadili na kutoa maamuzi mbalimbali na mapendekezo pale inapobidi.
d) Kuchagua wajumbe watatu wa Halmashauriya Kata/Wadi
e) Kuchagua wajumbe wawili watakaowakilisha Kata/Wadi kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya.
f) Kuhakikisha uhai wa Chama katika Kata/Wadi.
g) Kupokea ripoti za maendeleo, kutoka kwenye mikutano mikuu ya Kata/Wadi yaliyoko katika Kata/Wadi, na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maelekezo kwa Halmashauriya kila Tawi/Shehia.
h) Kutayarisha ripoti ya maendeleo ya wanachama/wananchi, ikionyesha hali halisi ya ajira (walioajiriwa na waliojiajiri) na kipato cha kaya, kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Jimbo/Wilaya.
i) Kupokea maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya.
j) Kupendekeza majina mawili ya wagombea wa Chama cha MAKINI katika uchaguzi wa diwani wa Kata/Wadi kwa Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya.
k) Kupendekeza jina la mgombea ubunge wa Chama cha MAKINI kutoka kwenye Kata/Wadi.
l) Kuwawajibisha viongozi wa Chama katika ngazi za Tawi/Shehia ambao watapatikana na makossa yanayostahili hatua za kinidhamu.

## 16.2 Halmashauriya Kata/Wadi

a) Kutakuwa na Halmashauriya Kata/Wadi itakayokutana si chini ya mara tatu kwa mwaka, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-
    i. Mwenyekiti wa Kata/Wadi
    ii. Katibu mtendaji wa Kata/Wadi
    iii. Mweka hazina wa Kata/Wadi
    iv. Wenyeviti wote wa Kata/Wadi yaliyomo katika Kata/Wadi
    v. Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi.
    vi. Diwani wa eneo la Kata/Wadi iwapo ni mwanachama wa MAKINI.
b) Koramu ya mkutano ya Halmashauriya Kata/Wadi itakuwa na nusu ya wajumbe wa Halmashauri waliotajwa katika kifungu 16.2 (a) (i) hadi (v)

### 16.2.1 Kazi ya Halmashauriya Kata au Wadi

a) Kusimamia shughuli zote za Chama, kuzitangaza, kuzitetea sera na ilani ya uchaguzi ya Chama, kushawishi wananchi wajiunge na Chama cha MAKINI, na kuboresha maendeleo ya wanachama/wananchi katika Kata/Wadi.

b) Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanachama/wananchi katika Kata/Wadi.

c) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya.

d) Kudumisha Amani, Umoja na mshikamano katika Kata/Wadi.

e) Kupokea ripoti za mikutano mikuu ya Kata/Wadi yaliyoko katika Kata/Wadi na kutathmini maendeleo ya Kata/Wadi, pamoja na kutoa mwelekezo wa baadaye kwa Halmashauriza Kata/Wadi

f) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kiuchumi, elimu, michezo n.k kwa kuwashirikisha wanachama/wananchi wenye kuhitaji huduma hizo.

g) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu wa Chama wa Jimbo/Wilaya.

h) Kuhimiza kila kaya kupelekea watoto shule, na kuhimiza wananchi kujiendeleza kielimu, ikiwa ni pamoja na kusaidia pale inapowezekana.

i) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka uliopita, na kutayarisha bajeti ya mwaka ya Chama, pamoja na ripoti za mapato na matumizi ya Chama katika Kata/Wadi.

j) Kusimamia matumizi bora ya mali ya Chama.

k) Kuunda kamati/idara mbalimbali za kufanikisha malengo ya Chama, hii ikiwa ni pamoja na kuteua wasimamizi wa kamati/idara hizo.

l) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuboresha demokrasia, hii ikiwa ni pamoja na kufanikisha chaguzi zote za kidomkrasia kwa kufanya kampeni kwa njia ya Amani.

m) Kuhitimisha maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Chama kwa Kata/Wadi, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya wanachama walio na sifa za kugombea nafasi za uongozi wa Chama katika Kata/Wadi.

n) Kupendekeza hatua za nidhamu kwa viongozi wa Kata/Wadi waliokiuka maadili ya uongozi, kwa ajili ya kufanyiwa uamuzi na Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi.

o) Kuteua jina la mweka hazina wa Kata/Wadi.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA

### VIKAO VYA JIMBO/WILAYA

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano kila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.

b) Kutakuwa na makamo Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.

c) Mwenyekiti wa Chama ndiye msemaji mkuu wa Chama, na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Chama katika Jimbo/Wilaya.

d) Makamu Mwenyekiti wa Chama atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti iwapo Mwenyekiti hatakuwepo.

e) Kutakuwa na katibu mtendaji wa Jimbo/Wilaya wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.

f) Kutakuwa na mweka hazina wa Jimbo/Wilaya ambae atateuliwa na Halmashauriya Jimbo/Wilaya.

g) Kutakuwa na Mkutano Mkuummoja kila mwaka chini ya Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya wa Chama, ama makamu Mwenyekiti iwapo Mwenyekiti hayupo.

h) Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya utajumuisha wajumbe wafuatao:-

  i. Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya
  ii. Makamo Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya
  iii. Katibu mtendaji wa Jimbo/Wilaya
  iv. Mweka hazina wa Jimbo/Wilaya
  v. Wenyeviti wote wa Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya.
  vi. Makatibu wote wa Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya
  vii. Wajumbe wawili kutoka katika kila katia watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata inayohusika.
  viii. Wenyeviti wa vitengo vya Chama katika Jimbo/Wilaya.
  ix. Madiwani wote walioko katika Jimbo/Wilaya ambao ni wanachama wa Chama cha MAKINI.
  x. Mbunge aliyekatika Jimbo/Wilaya na ambae ni mwanachama wa Chama cha MAKINI.

i) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 17.1 (b) (i) hadi (viii)

j) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya katibu kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

k) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yoyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

### 17.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya

a) Kuchagua Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya

b) Kuchagua makamo Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya

c) Kuchagua katibu mtendaji wa Jimbo/Wilaya

d) Kupokea ripoti za utendaji kutoka HalmashauriJimbo/Wilaya, kuzijadili na kutoa maamuzi mbalimbali na mapendekezo pale inapobidi.

e) Kuchagua wajumbe watatu wa HalmashauriJimbo/Wilaya

f) Kuchagua wajumbe wawili watakaowakilisha Jimbo/Wilaya kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa.

g) Kuhakikisha uhai wa Chama katika Jimbo/Wilaya.

h) Kupokea ripoti za maendeleo, kutoka kwenye mikutano mikuu ya Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya, na ripoti ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maelekezo kwa Halmashauriya kila Kata/Wadi.

i) Kupitisha ripoti ya maendeleo kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Wilaya/Mkoa.

j) Kupokea maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Wilaya/Mkoa.

k) Kuchagua wagombea wa Chama cha MAKINI katika uchaguzi wa diwani katika Serikaliza Kata/Wadi.

l) Kupokea mapendekezo ya majina ya wagombea ubunge wa Chama cha MAKINI kutoka kwenye Kata/Wadi na kupendekeza majina yasiyozidi matatu kwa uongozi wa Chama Wilaya/Mkoa, kila jina likiwa na namba ya kura alizopata.

m) Kuwawajibisha viongozi wa Chama katika ngazi ya Kata/Wadi ambao watapatikana na makossa yanayostahili hatua za kinidhamu.

### 17.2 Halmashauriya Jimbo/Wilaya.

a) Kutakuwa na Halmashauriya Jimbo/Wilaya itakayokutana si chini ya mara nne kwa mwaka, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya
ii. Makamo Mwenyekiti wa Jimbo/Wilaya
iii. Katibu mtendaji wa Jimbo/Wilaya
iv. Mweka hazina wa Jimbo/Wilaya
v. Wenyeviti wote wa Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya.
vi. Wenyeviti wote wa vitengo vya Chama wa Jimbo/Wilaya.
vii. Makatibu wote wa Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya
viii. Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya
ix. Wenyeviti wa vitengo vya Chama katika Jimbo/Wilaya.
x. Madiwani wote Jimbo/Wilayani ambao ni wanachama wa MAKINI.
xi. Mbunge wa Jimbo/Wilaya kama ni mwanachama wa Chama cha MAKINI.

vii. Makatibu wote wa Kata/Wadi zilizoko katika Jimbo/Wilaya
viii. Wajumbe watatu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu waJimbo/Wilaya
ix. Wenyeviti wa vitengo vya Chama katika Jimbo/Wilaya.
x. Madiwani wote Jimbo/Wilayani ambao niwanachama wa MAKINI.
xi. Mbunge waJimbo/Wilaya kama ni mwanachama wa Chama cha MAKINI.

b) Koramu ya mkutano wa Halmashauriya Jimbo/Wilaya itakuwa nusu ya wajumbe wa Halmashauriwaliotajwa katika kifungu 17.2 (a) (i) hadi (vii)

**17.2.1 Kazi za Halmashauriya Jimbo/Wilaya**

a) Kusimamia shughuli zote za Chama, kuzitangaza, kuzitetea sera na ilani ya uchaguzi ya Chama, kushawishi wananchi wajiunge na Chama cha MAKINI, na kuboresha maendeleo ya wanachama/wananchi katika Jimbo/Wilaya.
b) Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanachama/wananchi katika Jimbo/Wilaya.
c) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa JIMBO/WILAYA
d) Kudumisha Amani, Umoja na mshikamano katika Jimbo/Wilaya
e) Kupokea ripoti za mikutano mikuu ya Kata/Wadi yaliyoko katika Kata/Wadina kutathmini maendeleo ya Jimbo/Wilaya, pamoja na kutoa mwelekezo wa baadaye kwa Halmashauriza Kata/Wadi.
f) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kiuchumi, elimu, michezo n.k kwa kuwashirikisha wanachama/wananchi.
g) Kutoa ushauri na misaada ya aina mbalimbali kwa wanachama,wananchi wenye kuhitaji huduma hiyo.
h) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu waChama wa Jimbo/Wilaya.
i) Kuhimiza kila kaya kupelekea watoto shule, na kuhimiza wananchi kujiendeleza kielimu, ikiwa ni pamoja na kusaidia pale inapowezekana.
j) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka uliopita, na kutayarisha bajeti ya mwaka ya Chama, pamoja na ripoti za mapato na matumizi ya Chama katika Jimbo/Wilaya.
k) Kusimamia matumizi bora ya mali ya Chama.
l) Kuunda kamati/idara mbalimbali za kufanikisha malengo ya Chama, hii ikiwa ni pamoja na kuteua wasimamizi wa kamati/idara hizo.
m) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuboresha demokrasia, hii ikiwa ni pamoja na kufanikisha chaguzi zote za kidomkrasia kwa kufanya kampeni kwa njia ya Amani.
n) Kuhitimisha maandalizi ya Mkutano Mkuu waChamawa Jimbo/Wilaya, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya wanachama walio na sifa za kugombea nafasi za uongozi wa Chama katika Jimbo/Wilaya.
o) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti ya maendeleo kwenye Mkutano Mkuu waJimbo/Wilaya, kwa ajili ya Mkutano Mkuu waChama wa JIMBO/WILAYA

## SEHEMU YA KUMI NA NANE

**VIKAO VYA MKOA**

Hivi ni vikao vya ngazi ya tano kutoka chini. Wilaya/Mkoa utauwa na vikao vya aina mbili kama ifuatavyo:-

### 18.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.

b) Kutakuwa na makamo Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.

c) Mwenyekiti wa Chama ndiye msemaji mkuu wa Chama, na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Chama katika Mkoa

d) Makamu Mwenyekiti wa Chama atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti iwapo Mwenyekiti hatakuwepo.

e) Kutakuwa na katibu mtendaji wa Mkoa wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa MKOA kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.

f) Kutakuwa na mweka hazina wa Mkoa ambae atateuliwa na Halmashauriya Mkoa.

g) Kutakuwa na Mkutano Mkuummoja kila mwaka chini ya Mwenyekiti wa Mkoa, ama mwanachama aliyechaguliwa na huo Mkutano Mkuu wa Mkoa kukaimu nafasi hiyo kwa mda

h) Mkutano Mkuu wa Mkoa utajumuisha wajumbe wafuatao:-

   i. Mwenyekitiwa Mkoa
   ii. Makamo Mwenyekiti wa Mkoa
   iii. Katibu mtendaji wa Mkoa
   iv. Mweka hazina wa Mkoa
   v. Wenyeviti wote wa Majimbo/Wilaya yaliyomo katika Mkoa.
   vi. Makatibu wote wa Majimbo/Wilaya yaliyoko katika Mkoa
   vii. Wajumbe wawili kutoka katika kila Jimbo/Wilaya watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo/Wilaya linalohusika.
   viii. Wenyeviti wa vitengo vya Chama katika Mkoa.
   ix. Madiwani wote Mkoa ni ambao ni wanachama wa MAKINI.
   x. Wabunge wote katika ambao ni wanachama wa MAKINI.

i) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Mkoa ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 18.1 (h) (i) hadi (viii)

j) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya katibu kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.

i) Koramu ya Mkutano Mkuu waMkoa ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 18.1 (h) (i) hadi (viii)
j) Wajumbe waMkutano Mkuu waMkoa watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya katibu kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.
k) Wajumbe wa Mkutano Mkuu waMkoa watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yoyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo kama Mwenyekiti na makamu wake watakuwa hawapo.

**18.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu waMkoa.**

a) Kuchagua MwenyekitiwaChama wa Mkoa.
b) Kuchagua makamo MwenyekitiwaChama wa Mkoa.
c) Kuchagua katibu mtendaji waMkoa.
d) Kupokea ripoti za utendaji kutoka Halmashauriya Mkoa,na ripoti ya utekelezaji wa ila ni ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maamuzi mbalimbali na mapendekezo pale inapobidi.
e) Kuchagua wajumbe watatu waHalmashauriya Mkoa.
f) Kuchagua mjumbe mmoja atakayewakilisha Mkoa kwenye Mkutano Mkuu waTaifa.
g) Kuhakikisha uhai waChama katika Mkoa.
h) Kupokea ripoti za maendeleo, kutoka kwenye mikutano mikuu ya Majimbo/Wilayayaliyoko katika Wilaya/Mkoa, na ripoti ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maelekezo kwa Halmashauriya kila Jimbo/Wilaya.
i) Kupitisha ripoti ya maendeleo ya Mkoakwa ajili ya Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa.
j) Kupokea maamuzi ya Halmashauri Kuu ya Taifa.
k) Kupokea mapendekezo ya majina ya wagombea ubunge waChama cha MAKINI kutoka katika Majimbo/Wilaya na kuwasilisha majina hayo makao makuu ya ChamaTaifa.
l) Kuwawajibisha viongozi waChama katika ngazi ya Majimbo/Wilaya ambao watapatikana na makossa yanayostahili hatua za kinidhamu.

**18.2 Halmashauriya Mkoa.**

a) Kutakuwa na Halmashauriya Mkoa itakayokutana si chini ya mara nne kwa mwaka, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-
   i. Mwenyekiti wa Mkoa
   ii. Makamo Mwenyekiti waMkoa
   iii. Katibu mtendaji wa Mkoa
   iv. Mweka hazina wa Mkoa
   v. Wenyeviti wote waMajimbo/Wilayayaliyoko katika Wilaya/Mkoa.

b) Koramu ya mkutano wa Halmashauriya Mkoa itakuwa nusu ya wajumbe wa Halmashauriwaliotajwa katika kifungu 18.2 (a) (i) hadi (viii)

**18.2.1 Kazi za Halmashauri ya Mkoa.**

a) Kusimamia shughuli zote za Chama, kuzitangaza, kuzitetea sera na ilani ya uchaguzi ya Chama, kushawishi wananchi wajiunge na Cham cha MAKINI, na kuboresha maendeleo ya wanachama/wananchi katika Wilaya/Mkoa.

b) Kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanachama/wananchi katika Mkoa.

c) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

d) Kudumisha Amani, Umoja na mshikamano katika Mkoa.

e) Kupokea ripoti za mikutano mikuu ya Majimbo/Wilaya yaliyoko katika Mkoa na kutathmini maendeleo ya Mkoa, pamoja na kutoa mwelekezo wa baadaye kwa Halmashauriza Majimbo/Wilaya.

f) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kiuchumi, elimu, michezo n.k kwa kuwashirikisha wanachama/wananchi.

g) Kutoa ushauri na misaada ya aina mbalimbali kwa wanachama,wananchi wenye kuhitaji huduma hizo.

h) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu wa Mkoa.

i) Kupokea ripoti za maendeleo ya sayansi, teknolojia, elimu, afya, lishe, ajira na kipato cha kaya kutoka kila Jimbo/Wilaya na kutayarisha takwimu za sekta hizo katika Mkoa kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Mkoa.

j) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka uliopita, na kutayarisha bajeti ya mwaka ya Chama, pamoja na ripoti za mapato na matumizi ya Chama katika Mkoa.

k) Kusimamia matumizi bora ya mali ya Chama.

l) Kuunda kamati/idara mbalimbali za kufanikisha malengo ya Chama, hii ikiwa ni pamoja na kuteua wasimamizi wa kamati/idara hizo na kupanga utaratibu wa utendaji wa kamati/idara hizo.

m) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuboresha demokrasia, hii ikiwa ni pamoja na kufanikisha chaguzi zote za kidomkrasia kwa kufanya kampeni kwa njia ya Amani.

n) Kuhitimisha maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Mkoa, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya wanachama walio na sifa za kugombea nafasi za uongozi wa Chama katika Mkoa.

m) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti ya maendeleo ya Mkoa kwenye Mkutano Mkuu wa Wilaya/Mkoa, kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

o) Kupendekeza hatua za kinidhamu kwa viongozi wa Majimbo/Wilaya walio na makosa yanayostahili hatua za kinidhamu, kwa ajili ya kufanyikwa uamuzi na Mkutano Mkuu wa Mkoa.

p) Kupokea na kuskiliza rufani za hatua za kinidhamu zilizochukuliwa na vikao vya Majimbo/Wilaya.
q) Kuthibitisha wenyeviti na Makatibu wa kitengo cha wataalam katika Mkoa.
r) Kuteua mweka hazina wa Mkoa.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA

## VIKAO VYA TAIFA

Hivi ni vikao vya ngazi ya sita na ya mwisho kutoka chini. Kutakuwa na vikao vya aina nne katika ngazi ya Taifa kama ifuatavyo.

### 19.1 Mkutano Mkuu wa Taifa

a) Kutakuwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.
b) Kutakuwa na Makamo Wenyekiti wa Taifa wa Chama (Tanzania Bara/Zanzibar), ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu kila baada ya miaka mitano,na anaweza kuchaguliwa tena.
c) Mwenyekiti wa Chama ndiye msemaji mkuu wa Chama, na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Chama katika Taifa, akisaidiwa na makamo wake wawili.
d) Makamu Mwenyekiti wa Chama (Tanzania Bara/Zanzibar) atatekeleza majukumu ya Mwenyekiti iwapo Mwenyekiti hatakuwepo.
e) Mkutano Mkuu Taifa utajumuisha wajumbe wafuatao:-
i) Mwenyekiti wa Chama Taifa
ii) Makamu Mwenyekiti (Tanzania Bara)
iii) Makamu Mwenyekiti (Tanzania Zanzibar)
iv) Katibu Mkuu wa Chama Taifa.
v) Naibu Katibu Mkuu (Tanzania Bara)
vi) Naibu Katibu Mkuu (Tanzania Zanzibar)
vii) Mweka Hazina wa Chama Taifa.
viii) Wenyeviti wote wa Mikoa
ix) Makatibu wote wa Mikoa
x) Mjumbe mmoja aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa kuwakilisha Mkutano Mkuu wa Taifa
xi) Wajumbe kumi na mbili wa Halmashauri Kuu ya Taifa.
xii) Wajumbe wanne wakuteuliwa na Mwenyekiti Taifa.
xiii) Wenyeviti na Makatibu wa vitengo vya chama ngazi ya Taifa.
xiv) Wakuu wa Idara/Kamati za chama.

f) Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Taifa wa Chama, ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuukila baada ya miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena.
g) Koramu ya Mkutano Mkuu wa Mkoa ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika kifungu 19.1 (e) (i) hadi (xiv)
h) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yeyote kukaimu nafasi ya Katibu Mkuu ama nafasi ya Naibu Katibu Mkuu kwa muda kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo.
i) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa watakuwa na haki ya kumchagua mwanachama yoyote kukaimu nafasi ya Mwenyekiti kwa muda huo kwa wingi wa kura ya wajumbe waliopo kama Mwenyekiti na makamu wake watakuwa hawapo.

**19.1.1 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa.**

a) Kufanya marekebisho katika Katiba ya Chama, na kupitisha marekebisho hayo kwa kura isiyopungua theluthi mbili ya wanachama wote waliotajwa katika kifungu 19.1 (e) (i) hadi (xiv)
b) Kuchagua Mwenyekiti wa Taifa
c) Kuchagua Makamo Mwenyekiti (Tanzania bara) na Makamu Mwenyekiti (Zanzibar)
d) Kuchagua Katibu Mkuu Taifa
e) Kupokea ripoti ya utendaji kutoka Halmashaurikuu ya Taifa, na ripoti ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama, kuzijadili na kutoa maamuzi mbalimbali na mapendekezo pale inapobidi.
f) Kuchagua wajumbe kumi na mbili wa Halmashauri kuu ya Taifa.
g) Kuwawajibisha viongozi wa chama katika ngazi ya Mkoa na Taifa ambao watapatikana na makosa yanayostahili hatua za kinidhamu.
h) Kuhakikisha uhai wa Chama Kitaifa.

**19.2 Halmashauri Kuu ya Taifa.**

a) Kutakuwa na Halmashauri ya Taifa itakayokutana si chini ya mara moja kwa mwaka, Mwenyekiti wa Taifa anaweza kutisha Halmashauri Kuu ya Taifa kwa zarura, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-
   i. Mwenyekiti wa chama Taifa.
   ii. Makamo Mwenyekiti wa Taifa(Tanzania Bara)
   iii. Makamo Mwenyekiti wa Taifa(Zanzibar)
   iv. Katibu Mkuu wa chama Taifa.
   v. Naibu Makatibu Wakuu (Bara na Zanzibar)
   vi. Mweka hazina wa chama Taifa na Naibu mweka hazina.
   vii. Katibu Mwenezi na Naibu Katibu Mwenezi Taifa.
   viii. Wajumbe kumi na mbili waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.
   ix. Wenyeviti na Makatibu wa vitengo vya chama, ngazi ya Taifa.

x. Wajumbe wanne watakao teuliwa na Mwenyekiti Taifa

xi. Wakuu wa Idara za chama.

b) Koramu ya mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa nusu ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

**19.2.1 Kazi za Halmashauri Kuu ya Taifa.**

a) Kusimamia:

i) Shughuli zote za chama Kitaifa na kupanga taratibu za utendaji katika ngazi zote za uongozi katika chama.

ii) Utekekelezaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanachama Kitaifa.

iii) Utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

b) Kuchagua Manaibu Katibu Wakuu wa Taifa.

c) Kuteua Mweka Hazina na Naibu mweka Hazina wa Taifa.

d) Kuteua Katibu Mwenezi na Naibu Katibu Mwenezi wa Taifa.

e) Kupokea ripoti za mikutano mikuu ya Mikoa, kutathmini maendeleo ya Taifa, na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama, na kutoa mwelekeo wa baadaye kwa Halmashauri za mikoa.

f) Kuteua jina la mgombea majina mawili ya wagombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania, na majina mawili ya wagombe wa kiti cha Uria wa Zanzibar.

g) Kudumisha Amani, Umoja na mshikamano katika Taifa.

h) Kutunga sera za chama na ilaani ya uchaguzi ya chama kuwa vitendo vya maendeleo ya wanachama/wananchi, na kutoa mapendekezo katika ngazi zote za chama.

i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kiuchumi, elimu, michezo, n.k kwa kuwashirikisha wanachama/wananchi.

j) Kutoa ushauri na misaada ya aina mbalimbali kwa wananchi/wanachama wenye kuhitaji huduma hizo.

k) Kuwasilisha matatizo ya wanachama/wananchi katika Mkutano Mkuu wa Taifa.

l) Kupokea ripoti za maendeleo ya sayansi, teknolojia, elimu, afya, lishe, ajira nakipato cha kaya kutoka kila Wilaya/Mkoa na kutayarisha takwimu za sekta hizo Kitaifa kwa ajili ya Mkutano Mkuu wa Taifa

m) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa mwaka uliopita, na kutayarisha bajeti ya mwaka ya Chama, pamoja na ripoti za mapato na matumizi ya Chama Kitaifa.

n) Kusimamia matumizi bora ya mali ya Chama.

o) Kuunda kamati/idara mbalimbali za kufanikisha malengo ya Chama, hii ikiwa ni pamoja na kuteua wasimamizi wa kamati/idara hizo na kupanga utaratibu wa utendaji wa kamati/idara hizo.

p) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuboresha demokrasia, hii ikiwa ni pamoja na kufanikisha chaguzi zote za kidomkrasia kwa kufanya kampeni kwa njia ya Amani.

q) Kuhitimisha maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya wanachama walio na sifa za kugombea nafasi za uongozi wa Chama katika ngazi ya Wilaya/Mkoa.

r) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti ya maendeleo kwenye Mkutano Mkuu wa Taifa.

s) Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi wa chama katika ngazi ya Wilaya/Mkoa na Taifa ambao watapatikana na makossa yanayostahili hatua za kinidhamu.

t) Kukubali ama kukataa maombi ya wanachama wanaotaka kujiunga na chama baada ya kupoteza uanachama wao.

u) Kupokea kusikiliza rufani za hatua za kinidhamu zilizochukuliwa na vikao vya mikoa.

v) Kuteua wajumbe sita wa Kamati Kuu ya Taifa.

w) Kuteua majina ya wagombea wa chama cha makini haitka uchaguzi wa wabunge.

x) Kuteua wajumbe wane wa baraza la wadhamini wa chama na kusimamia shughuli za baraza hilo.

y) Kuwasilisha ripoti ya mapato na matumizi ya chama kwa Mwenyekiti wa baraza la wadhamini mara moja kila mwaka.

z) Kufanya marekebisho ya chama, Halmashaauri kuu ya Taifa itakaa kama kamati maalum kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa chama Taifa na kufanya kazi zote za Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

aa) Kuwasilisha bajeti ya chama kwa Mwenyekiti wa baraza la wadhamini wa chama kwa ajili ya kupata kibali cha mwisho cha kutumia bajeti hiyo.

**19.3 Kamati Kuu ya Taifa.**

Kutakuwa na Kamati Kuu ya Taifa itakayokutana si chini ya mara mbili kwa mwaka, na itakayokuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa chama Taifa, ambaye pia atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Kamati Kuu na anaweza kuitisha cha dharura.
ii. Makamu Mwenyekiti wa Taifa(Tanzania Bara)
iii. Makamu Mwenyekiti wa Taifa(Zanzibar)
iv. Katibu Mkuu wa chama Taifa.
v. Naibu Katibu Mkuu(Tanzania Bara)
vi. Naibu Katibu Mkuu(Zanzibar)
vii. Katibu Mwenezi na Naibu Katibu Mwenezi wa Taifa.
viii. Mweka Hazina na Naibu mweka Hazina wa Taifa.
ix. Wajumbe sita watakaoteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.
x. Wakuu wa Idara za chama.

**19.3.1 Kazi za Kamati Kuu ya Taifa.**

a) Kuratibu shughuli zote za chama Kitaifa.
b) Kutoa taarifa za kukipatia chama mapato na kusimamia utekelezaji wa taratibu hizo, hii ikiwa ni pamoja na kupanga viwango vya ada ya uanachama mara kwa mara, kubuni miradi ya kukipatia chama mapato, na kutafuta wafadhii wa chama.
c) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza nyaraka mbalimbali kwa lengo la kuwaelimsha wananchi juu ya haki zao kwa Serikalina chama, na majukumu yao katika maendeleo ya Taifa.
d) Kuteua wajumbe wa Sekretarieti ya chama Taifa.
e) Kufanya kazi nyingine zozote itakayopangiwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

**9.4 Sekretarieti ya chama.**

A. Kutakuwa na Sekretarieti ya chama itayokutana wakati wowote.
a. Katibu Mkuu wa chama Taifa ambaye pia atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya sekretarieti.
b. Naibu Makatibu wakuu Bara na Zanzibar Taifa mmoja wapo atakuwa ni Katibu wa Sekretarieti.
c. Wakuu wa Idara/Kamati za chama.
d. Katibu Mwenezi na Naibu Katibu Mwenezi Taifa.
e. Mweka hazina na Naibu Mweka Hazina Taifa.
f. Sekretarieti watakuwa na mamlaka ya kuteua wanachama wenye sifa za uchapakazi kushiriki katika shughuli za idara husika.

**19.4.1 Kazi za viongozi wa Idara za Sekretarieti.**

a) Kuratibu maendeleo ya wanachama katika idara zilizotajwa.
b) Kutayarisha agenda ya mikutano yote ambayo Mwenyekiti wake ni Mwenyekiti wa chama Tifa.
c) Kubuni mbinu za kuleta maendeleo ya haraka katika idara zilizotajwa.
d) Kufuatilia mwenendo wa Serikali iliyoko madarakani na kutoa ushauri pale ambapo inabidi.
e) Kufanya kazi nyingine kama zitakavyopangiwa na Mwenyekiti wa Sekretarieti.

## SEHEMU YA ISHIRINI

**VIONGOZI WAKUU WA CHAMA.**

20. Viongozi wakuu wa chama ni:-

a) Mwenyekiti wa Chama Taifa.
b) Makamu wenyeviti wa Chama Taifa.
c) Katibu Mkuu wa chama Taifa.
d) Naibu Makatibu Wakuu wa Chama Taifa.
e) Mweka hazina na Naibu mweka hazina Taifa.
f) Katibu Mwenezi na Naibu Katibu mwenezi Taifa.

**MWENYEKITI**

a) Atakuwa msemaji na mhamasishaji mkuu wa chama, na ataongoza vikao vyote vya Taifa.
b) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kura ya siri, na atatakiwa kupata si chini ya theluthi mbili ya kura zote zitakazopigwa na ambazo hazikuharibika.
c) Atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Halmashauri Kuu ya Taifa na Kamati Kuu, isipokuwa vikao vya kuchagua Mwenyekiti Taifa.
d) Vikao vya kuchagua Mwenyekiti wa chama Taifa vitaongozwa na wanachama watakaochaguliwa, miongoni mwa wajumbe waliohudhuria, kwa kura isiyopungua theluthi mbili.
e) Atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano, na anaweza kuchaguliwa tena baada ya kipindi hicho kumaliza.
f) Ataondolewa madarakani kabla ya muda wake kuisha kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa, ambalo limepitishwa na si chini ya theluthi mbili ya kura za siri za wajumbe wote wa mkutano mkuu, baada ya kupokea matokeo ya kura za maoni kutoka Halmashauri za Majimbo/Wilaya yote zikionyesha kwa asilimia isiyopungua theluthi mbili kuwa hafai.

**MAKAMU MWENYEKITI**

a) Makamu Mwenyekiti kutoka (Zanzibar) atafanya shughuli za chama Tanzania Zanzibar, na Makamu Mwenyekiti (Tanzania Bara) atafanya shughuli za chama Tanzania Bara, isipokuwa watakavyoelekezwa na Mwenyekiti kufanya shughuli zao sehemu nyingine.
b) Watakuwa wasaidizi wa Mwenyekiti wa chama Taifa.
c) Watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa, kwa kura ya siri isiyopungua theluthi mbili ya kura zote zilizopigwa na ambazo hazikuharibika.
d) Watashika madaraka kwa miaka mitano, na watakuwa na haki ya kugombea tena baada ya kipindi hicho kumaliza.
e) Wataweza kuondolewa kwenye madaraka, kabla ya muda wao kumaliza, kwa azimio la Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa, ambalo limepitishwa na si chini ya theluthi mbili ya kura za siri za wajumbe wa mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa, baada ya kupokea pendekezo la kuondolewa madarakani kutoka kwa Kamati Kuu ya chama.
f) Watafanya kazi zote za chama kama watakavyopangiwa na Mwenyekiti wa chama Taifa.

**KATIBU MKUU**

a) Atachaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano mkuu wa taifa kwa kura uya siri isiyopungua theluthi mbili ya kura zote ziliopigwa, na ambazo hazikuharibika.
b) Atakuwa katibu wa vikao vyote vitakavyoongozwa na Mwenyekiti wa chama Taifa.
c) Atakuwa mtendaji na msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Chama.
d) Atakuwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Chama.
e) Atatayarisha nyaraka zote za mikutano ya Halmashauri Kuuya Taifa, Kamati Kuu ya Taifa, na mikutano mingine kama akavyoelekezwa na Mwenyekiti wa chama Taifa.
f) Ataweza kuondolewa kwenye madaraka kabla ya muda wake kumalizika, kwa azimio la Mkutano MKuu wa Taifa, ambalo limepitishwa na si chini ya theluthi mbili ya kura za siri za wajumbe wote wa Mkutano Mkuu, baada ya kupokea pendekezo la kuondolewa madarakani kutoka kwa Kamati Kuu ya chama.
g) Atafanya kazi nyingine zote atakazopangiwa na Mwenyekiti wa chama Taifa.
h) Atashika madaraka kwa miaka mitano, na atakuwa na haki ya kugombea tena baada ya kipindi hicho kumaliza.

**NAIBU MAKATIBU WAKUU**

a) Watachaguliwa na wajumbe wa Mkutano Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka miongoni mwao kwa kura isiyopungua theluthi mbili ya kura zote zilizopigwa, na ambazo hazikuharibika.
b) Katibu Mkuu atamteua Naibu Katibu Mkuu mmoja wapo kukaimu nafasi yake pale ambapo atakuwa hayupo
c) Watafanya kazi nyingine zote watakazopangiwa na Katibu Mkuu au Kamati Kuu.
d) Watashika madaraka kwa miaka mitano, na watakuwa na haki ya kugombea tena baada ya kipindi hicho kumaliza.
e) Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar) atafanya kazi za chama Tanzania Zanzibar, na Naibu Katibu Mkuu (Tanzania Bara) atafanya kazi za chama Tanzania bara, isipokuwa pale watakapopangiwa vinginevyo na Katibu Mkuu.
f) Ataweza kuondolewa kwenye madaraka kabla ya muda wake kumalizika, kwa azimio la Halmashauri Kuu ya Taifa, ambalo limepitishwa na si chini ya theluthi mbili ya kura za siri za wajumbe wote wa Halmashauri kuu, baada ya kupokea pendekezo la kuondolewa madarakani kutoka kwa Kamati Kuu ya chama.

**20.5 Mweka Hazina /Naibu Mweka Hazina Taifa**

a) Watateuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa
b) Watatoa taarifa za mapato na matumizi ya Chama kwenye mikutano yote ya Halmashauri Kuu ya Taifa.
c) Watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano, na wanaweza kuteuliwa tena baada ya kipindi hicho kumalizika.

d) Wanaweza kuondolewa madarakani kabla ya muda wao kuisha na mkutano wa Halmashari Kuu baada ya kuthibitika wamekoso sifa ya utendaji kazi zao kutoka Kamati Kuu Taifa.

**20.6 Katibu Mwenezi na Naibu Katibu Mwenezi Taifa**

a) Watateuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa
b) Wataeneza Sera, Ilani, Mikakati na Program za chama zitakazokwisha amriwa na chama.
c) Watasambaza taarifa mbali mbali za chama kama watakavyo pangiwa na viongozi wa Kitaifa na Vikao vya chama.
d) Watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na wanaweza kuteuliwa tena baada ya muda wake kumalizika.
e) Wanaweza kuondolewa madarakani kabla ya muda wao kuisha na mkutano wa Halmashari Kuu baada ya kuthibitika wamekoso sifa ya utendaji kazi zao kutoka Kamati Kuu Taifa.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA

## WAGOMBEA WA KITI CHA URAIS

21.1 Wagombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

a) Wawe wametimiza masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanayohusu mgombea wa kiti cha urais.
b) Wawe wanachama wa Chama cha MAKINI.
c) Halmashauri Kuu ya Chama Taifa itachagua mgombea mmoja, miongoni mwa wagombea wawili mwa wagombea waliojitokeza, baada ya kusikiliza kila mgombea akizieleza sifa alizo nazo, pamoja na maelezo ya kina ya sababu za kugombea kiti hicho.
d) Kabla ya kupigiwa kura, kila mgombea wa kiti cha Urais ni lazima apendekeze jina la atakayekuwa mgombea mwenza wake, wakati wa kampeni za Urasi, kwa Kamati Kuu ya Taifa. Mgombea kiti cha Urais ana haki ya kutajwa na mgombea mwingine kama mgombea mwenza.

**21.2 Wagombea wa kiti cha Urais wa Tanzania Zanzibar.**

a) Wawe wametimiza masharti ya Katiba ya Zanzibar yanayohusu mgombea wa kiti cha Urais wa Zanzibar.
b) Wawe wanachama wa Chama cha MAKINI.
c) Halmashauri Kuu ya Taifa wa itachagua mgombea mmoja, miongoni mwa wagombea wawili kama watakavyopendekezwa na Kamati Kuu, baada ya kusikiliza kila mgombea akizieleza sifa alizo nazo, pamoja na maelekezo ya kina ya sababu za kugombea kiti hicho.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI

**VITENGO VYA CHAMA**

Chama kitakuwa na Vitengo vifuatavyo:-

a) Kitengo cha Umoja wa Vijana
b) Kitengo cha Umoja wa Wanawake
c) Kitengo cha Umoja wa Walemavu
d) Kitengo cha Umoja wa Wazee
e) Kitengo cha Umoja wa Wataalam

### 22.1 KITENGO CHA UMOJA WA VIJANA

a) Kutakuwa na kitengo cha Umoja wa vijana wa chama, kitakachojishughulisha na maendeleo ya vijana, na mikakati ya kushirikisha vijana katika kufanikisha sera za chama na ilani ya uchaguzi.

b) Katika chama cha makini, kijana ni mtanzania aliye na umri wa miaka kumi na nane hadi miaka arobaini na tisa, na kijana yoyote mwanachama wa makini ana haki ya kuwa mwanachama wa kitengo cha Umoja wa vijana.

c) Wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi za Jimbo/Mkoa na Taifa watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa vijana katika ngazi husika, kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya kura zilizopigwa na ambazo hazikuharibika.

d) Kutakuwa na Halmashauri za Umoja wa vijana katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.1 (c) ambazo zitaongozwa na wenyeviti husika.

e) Wenyeviti na Makatibu wa Umoja wa vijana katika ngazi ya Jimbo/Mkoa na Taifa watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri ya Taifa ya Umoja wa vijana.

f) Mwenyekiti wa Umoja wa vijana katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya chama katika ngazi husika. Kwa mfano, Mwenyekiti wa Umoja wa vijana Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri Kuuya chama Taifa.

g) Halmashauri ya Umoja wa Vijana Taifa itatunga kanuni na taratibu za kuendesha Umoja huo na kuziwasilisha kwa Kamati Kuu ya Taifa kwa kuidhinishwa, isipokuwa kwa kuanzia shughuli za kuunda Umoja huo zitakuwa jukumu la Kamati Kuu ya Taifa.

h) Miongoni mwa shughuli za kitengo cha Umoja wa vijana katika kila ngazi iliyotajwa katika kifugnu 22.1 (c) ni kuhakikisha kuwa kila kijana katika ngazi hiyo anapatiwa elimu inayolingana na wezo wake, kuhakikisha kuwa haki za binaadamu zinazingatiwa kikamilifu, na kuhakikisha kuwa vijana wanasaidiwa katika harakati zao za kutafuta ajira.

### 22.2 KITENGO CHA UMOJA WA WANAWAKE

a) Kutakuwa na kitengo cha Umoja wa wanawake wa chama kitakachojishuhulisha na maendeleo ya wanawake, na mikakati ya kushirikisha wanawake katika kufanikisha sera za chama na ilani ya uchaguzi.

b) Mwanamke yoyote aliye mwanachama wa makini ana haki ya kuwa mwanachama wa kitengo cha Umoja wa wanawake.
c) Wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi za Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa wanawake katika ngazi husika, kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya kura zilizopigwa na ambazo hazikuharibika.
d) Kutakuwa na Halmashauri za Umoja wa wanawake, katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.2 (c) ambazo zitaongozwa na wenyeviti husika.
e) Wenyeviti na Makatibu wa Umoja wa wanawake katika ngazi ya Wilaya/Mkoa na Taifa watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri ya Taifaya Umoja wa wanawake.
f) Mwenyekiti wa Umoja wa wanawake katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya chama katika ngazi husika. Kwa mfano, Mwenyekiti wa Umoja wa wanawake Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama Taifa.
g) Kitengo cha Umoja wa wanawake Taifa kitatunga kanuni na taratibu za kuendesha Umoja huo, na kuziwasilisha kwenye Kamati Kuu ya Taifa kwa kuidhinishwa, isipokuwa kwa kuanzia shughuli za kuunda Umoja huo zitakuwa jukumu la Kamati Kuu ya Taifa.
h) Miongoni mwa shughuli za kitengo cha Umoja wa wanawake katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.2 (c) na kuhakikisha kuwa kila mwanamke katika ngazi hiyo anapatiwa elimu inayolingana na uwezo wake, na kuhakiksiha kuwa haki za wanawake zinatekelezwa kikamilifu.

## 22.3 KITENGO CHA UMOJA WALEMAVU

a) Kutakuwa na kitengo cha Umoja walemavu wa chama, kitakachojishughulisha na maendeleo ya walemavu, na mikakati ya kushirikisha walemavu katika kufanikisha sera za chama na ilani ya uchaguzi.
b) Katika chama cha MAKINI, mlemavu ni mtanzania aliye na umri wa miaka kumi na nane hadi miaka arobaini na tisa, na walemavu yoyote mwanachama wa makini ana haki ya kuwa mwanachama wa kitengo cha Umoja wa walemavu.
c) Wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi za Jimbo/Wilaya/Mkoa, na Taifa watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa walemavu katika ngazi husika, kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya kura zilizopigwa na ambazo hazikuharibika.
d) Kutakuwa na Halmashauri za Umoja wa walemavu katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.1 (c) ambazo zitaongozwa na wenyeviti husika.
e) Wenyeviti na Makatibu wa Umoja wa walemavu katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri ya Taifa ya Umoja wa walemavu.
f) Mwenyekiti wa Umoja wa walemavu katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya chama katika ngazi husika. Kwa mfano,

Mwenyekiti wa Umoja wa walemavu Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama Taifa.

g) Halmashauri ya Umoja wa walemavu Taifa itatunga kanuni na taratibu za kuendesha Umoja huo na kuziwasilisha kwa Kamati Kuu ya Taifa kwa kuidhinishwa, isipokuwa kwa kuanzia shughuli za kuunda Umoja huo zitakuwa jukumu la Kamati Kuu ya Taifa.

h) Miongoni mwa shughuli za kitengo cha Umoja wa walemavu katika kila ngazi iliyotajwa katika kifugnu 22.1 (c) ni kuhakikisha kuwa kila mlemavu katika ngazi hiyo anapatiwa elimu inayolingana na wezo wake, kuhakikisha kuwa haki za binaadamu zinazingatiwa kikamilifu, na kuhakikisha kuwa walemavu wanasaidiwa katika harakati zao za kutafuta ajira.

## 22.4 KITENGO CHA UMOJA WA WAZEE

a) Kutakuwa na kitengo cha Umoja wa wazee wa chama kitakachojishughulisha na maendeleo ya wazee, na mikakati ya kushirikisha wazee katika kufanikisha sera za chama na ilani ya uchaguzi.

b) Katika chama cha makini, mzee ni mtanzania aliye na umri wa miaka inayozidi arobaini na tisa, na mzee yeyote mwanachama wa makini ana haki ya kuwa mwanachama wa kitengo cha Umoja wa wazee.

c) Wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi za Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifawatachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa wazee katika ngazi husika, kwa kura zisizopungua theluthi mbili ya kura zilizopigwa na ambazo hazikuharibika.

d) Kutakuwa na Halmashauri za Umoja wa wazee, katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 23.2 (c) ambazo zitaongozwa na wenyeviti husika.

e) Wenyeviti na Makatibu wa Umoja wa wazee katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa watakuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri ya Taifa ya Umoja wa wazee.

f) Mwenyekiti wa Umoja wa wazee katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa atakuwa mjumbe wa Halmashauri ya chama katika ngazi husika. Kwa mfano, Mwenyekiti wa Umoja wa wazee atakuwa mjumbe Jimbo/Wilaya/Mkoa wa Halmashauri Kuu ya chama Jimbo/Wilaya/Mkoa

g) Kitengo cha Umoja wa wazee Taifa kitatunga kanuni na taratibu za kuendesha Umoja huo, na kuziwasilisha kwenye Kamati Kuu ya Taifakwa kuidhinishwa, isipokuwa kwa kuanzia shughuli za kuunda Umoja huo zitakuwa jukumu la Kamati Kuu ya Taifa.

h) Miongoni mwa shughuli za kitengo cha Umoja wa wazee katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.3 (c) ni kuhakikisha kuwa kila mila na desturi zinazotunzwa na kufuatwa, na matatizo ya wazee yanapatiwa ufumbuzi.

### 22.5 KITENGO CHA UMOJA WA WATAALAM

ii) Kutakuwa na kitengo cha Umoja wa wataalam wa chama kitakachojishughulisha na matumizi bora ya utaalam uliopo ndani nan je ya nchi, kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kisayansi, kiteknolojia na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

iii) Katika chama cha makini, mtaalam ni mtanzania aliye na umri wa miaka isiyopungua 18, aliyejiendeleza kielimu mpaka kikomo cha kipaji chake, na kudhihirisha kwa vitendo vipya au mawazo mapya kuwa ana uwezo mkubwa wa kutoa ushauri na huduma zitakazoleta mageuzi yanayokusudiwa na chama.

iv) Uanachama katika kitengo cha Umoja wa wataalam utakuwa kwa kuwasilisha maombi, kwa Halmashauri ya ngazi husika, na kupendekezwa na wanachama wasiopungua 10 katika ngazi ya Jimbo/Wilaya, 20 katika ngazi ya Wilaya/Mkoa na 25 katika ngazi ya Taifa, isipokuwa wanachama wa makini walio na shahada za falsafa katika fani yoyote hawatahitaji kupendekezwa.

v) Wenyeviti wa vitengo na wataalam katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.4 (c) watakuwa wajumbe wa Halmashauri, na washauri wa Mwenyekiti wa chama, katika ngazi husika

vi) Wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi ya Jimbo/Wilaya watapendekezwa na Halmashauri ya kitengo katika jumbo, na kuthibitishwa na Halmashauri ya chama Jimbo/Wilaya/Mkoa na wenyeviti na Makatibu wa kitengo katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa/Taifa watapendekezwa na Halmashauri ya kitengo katika Wilaya/Mkoa/Taifa, na kuthibitishwa na Kamati Kuu ya chama.

vii) Wenyeviti na Makatibu wa vitengo vya wataalam katika ngazi ya WILAYA/MKOA na Taifawatakuwa miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri ya Taifaya Umoja wa wataalam.

viii) Mwenyekiti wa Umoja wa wataalam katika ngazi ya Jimbo/Wilaya/Mkoa na Taifa atakuwa mjumbe na mmoja wa washauri wa Mwenyekiti wa chama katika ngazi husika. Kwa mfano, Mwenyekiti wa Umoja wa wataalam Taifa atakuwa mjumbe na mmoja wa washauri wa Mwenyekiti wa chama Taifa.

ix) Kitengo cha Umoja wa wataalam Taifakitatunga kanuni na taratibu za kuendesha Umoja huo, na kuziwasilisha kwenye Kamati Kuu ya Taifakwa kuidhinishwa, isipokuwa mwa kuanzia shughuli za kuunda Umoja huo zitakuwa jukumu la Kamati Kuu ya Taifa.

x) Miongoni mwa shughuli za kitengo cha Umoja wa wataalam katika kila ngazi iliyotajwa katika kifungu 22.4 (c) ni kuhakikisha kuwa utaalam unapewa hadhi inayokubalika kimaTaifa, kuwashawishi wataalam kutumia uwezo wao wote kuleta mapinduzi yanayokusudiwa na chama, na kudumisha mahusiano kati ya wataalam wa kitaanzania na wataalam kutoka pande zote za dunia.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU

**NAFASI ZIKIWA WAZI**

23.1 Iwapo nafasi ya uongozi itakuwa wazi katika ngazi yoyote ya uongozi wa chama ama vitengo vyake, nafasi hiyo itazibwa kwa haraka iwezekanavyo.

23.2 Nafasi za ngazi ya Kitaifa Kamati Kuu itakasimu madaraka ya Mkutano Mkuu ili kuziba haraka nafasi iliyo wazi.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE

**BARAZA LA WADHAMINI WA CHAMA**

24.1 Kutakuwa na baraza la wadhamini wa chama litakalokuwa na wajumbe wafuatao:-

i) Wajumbe wanne watakaoteuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

ii) Mwenyekiti wa baraza ambaye atateuliwa na wajumbe wa baraza.

24.2 Baraza litakuwa na haki ya kuyatumia mamlaka yake kama sharia ya nchi kuhusu wadhamini inavyoruhusu.

24.3 Baraza litakuwa na haki ya kuyatumia mamlaka ya kumiliki mali yote ya chama.

24.4 Baraza la wadhamini litafanya kazi zake kwa kusimamiwa na Halmashauri ya Taifa.

24.5 Muda wa kuwa mdhamini wa chama ni miaka mitano, lakini mdhamini aliyemaliza muda wake anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

24.6 Mjumbe anaweza kuondolewa katika Baraza la wadhamini na Halmashauri Kuu ya Taifa, baada ya kushauriwa na Kamati Kuu, ikiwa:-

i) Atakuwa mgonjwa, kwa muda usiopungua miezi sita, kiasi cha kumfanya ashindwe kufanya kazi zake.

ii) Atakuwa ameshindwa kufanya kazi zake kwa muda Zaidi ya miezi mine bila sababu zinazokubalika.

iii) Kama atakuwa amepoteza uanachama wake.

iv) Kama atakuwa amevunja sharia ya nchi kwa kutenda kosa la jinai, lisilokuwa la kisiasa.

v) Atafilisiwa.

24.7 Mdhamini atakuwa na haki ya kujiuzulu kwa utaratibu utakaotolewa na Kamati Kuu ya Taifa.

24.8 Nafasi ya mdhamini ikiwa wazi itajazwa mara moja kwa kufuata Katiba ya chama.

24.9 Iwapo Mwenyekiti wa baraza la wadhamini atashindwa kuhudhuria kikao chochote, wajumbe wa kikao watamchagua mmoja wao kukaimu nafasi ya Mwenyekiti katika kikao hicho.

24.10 Mwenyekiti wa Baraza atakuwa na haki ya kura ya turufu iwapo kura za wajumbe zitafungana baada ya kurudia mara mbili.

24.11Kamati Kuu ya Taifaitakuwa na mamlaka ya kusimamisha mdhamini, wadhamini ama baraza lote na kuwasilisha, kwa Halmashauri Kuuya Taifa, waraka unaooleza sababu za kuchukua hatua hiyo ili Halmashauri Kuuitoe uamuzi wa mwisho.

24.12 wajumbe wa baraza la wadhamini watakuwa na haki zifuatazo:

i) Kumtaka mwanachama yeyote binafsi au kikao chochote cha chama au afisa au mtendaji yeyote wa chama awasilishe riporti au taarifa yotote inayohusu chama kwa Mwenyekiti wa baraza.

ii) Kuhudhuria kikao chochote cha chama kama wasikilizaji.

24.13 Baraza la wadhamini litafanya kazi zifuatazo:-

a) Kusimamia na kudhibiti matumizi ya mali zote za chama zisizoondosheka na zinazoondosheka, pamoja na shughuli zote za kibiashara au miradi ya kiuchumi ya chama.

b) Kufanya shughuli zozote halali za uchumi kwa lengo la kuboresha mapato ya chama.

c) Kuunda kamati mbalimbali na kuzipa madaraka ya kutekeleza majukumu ya Baraza kwa niaba ya Baraza.

d) Kutoa taarifa ya utendaji yam waka katika kikao cha Halmashauri Kuuya Taifa.

e) Kupokea na kuchambua ripoti ya mapato na matumizo ya chama kwa Mwenyekiti wa baraza la wadhamini mara moja kila mwaka.

f) Kupokea bajeti ya chama na kutoa kibali cha mwisho cha kutumia bajeti hiyo.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO

### MAREKEBISHO YA KATIBA

25.1 Mkutano Mkuu wa Taifa/Halmashauri Kuu ya Taifa ndio wenye mamlaka ya kufanya marekebisho ya katiba, baada ya kupata mapendekezo ya Kamati Kuu ya Taifa.

25.2 Mabadiliko ya Katiba ni lazima yakubaliwe na theluthi mbili ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa/Halmashauri Kuu wenye haki ya kupiga kura.

### KANUNI ZA CHAMA

26.1 Kutakuwa na kanuni za chama zitakazotungwa na Halmashauri Kuu ya chama na zitaanza kutumika pale zitakapotiwa saini na Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama Taifa.

26.2 Kanuni hizi zitasaidia kazi ya Katiba na zitakuwa ndio mwongozo wa kusimamia Katiba katika kuleta tafsiri pale patakapo tokea mgongano.Tafsiri sahihi ya jambo hilo itapatikana katika Katiba ya Chama.

26.3 Halmashauri Kuu pekee ndio yenye uwezo wa kurekebisha Kanuni kwa kuongeza ama kupunguza kifungu chochote katika Kanuni hizi pale inapoona inafaa.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA

**KUVUNJA CHAMA**

27.1 Chama kinaweza kuvunjwa kwa azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa lililopitishwa si chini ya theluthi mbili ya wajumbe wa kikao hicho wenye haki ya kupiga kura.

27. 2 Pendekezo la kuvunja Chama nilazima liwasilishwe kwa wajuumbe wa Halmashauri Kuu si chini ya siku 120 kabla ya kuvunja Chama.

27.3 Baada ya Chama kuvunjwa, mali zote za Chama zitakabidhiwa kwa bodi ya Chama ili kufuata taratibu nyengine.

Marekebisho ya Katiba hii ni kutokana na mapendekezo yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa uliofanyika tarehe 20/06/2015.

Hivyo, toleo hili la Katiba la mwaka 2015 ndio Katiba itakayotumika katika Chama cha Demokrasia MAKINI na ndio mwongozo wa kusaidia utendaji kazi za Chama katika kukiletea Chama maendeleo.

**Katiba hii imetiwa sahihi leo tarehe 24TH May, 2016**

KATIBU MKUU TAIFA CHAMA CHA DEMOKRASIA MAKINI BOX ........ DAR ES SALAAM

MWENYEKITI WA TAIFA DEMOKRASIA MAKINI

**..........................**
**AMEIR H. AMEIR**
**KATIBU MKUU TAIFA**
**DEMOKRASIA MAKINI**

**..........................**
**MOHAMED ALI ABDULLA**
**MWENYEKITI TAIFA**
**DEMOKRASIA MAKINI**